# pspTB na matukio

Dodoma - Tanzania

Toleo Na 01- Januari - Juni 2025





# Matumizi ya kidijitali hayaepukiki sekta ya ununuzi na ugavi

Ujumbe wa Mkurugenzi Mtendaji

# Karibu Katika Toleo la Kwanza la Jarida la PSPTB

**Ndugu Msomaji,**

**Napenda kutambulisha katika toleo jipya kabisa la Habari na kukuhabarisha katika toleo jipya la jarida la PSPTB**.

PSPTB inayofuraha kukuletea chapisho ambalo lina lengo la kuhabarisha, kuhamasisha na kushirikisha umma katika kutekeleza majukumu yake katika kusimamia Ununuzi na ugavi nchini

Ni wajibu wetu kuufahamisha umma juu ya mipango yetu, mikakati yetu na maendeleo ya utekelezaji wa kazi zetu katika kufikia malengo tuliyojiwekea kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi.

Katika kufikia malengo yetu, tutahakikisha tunaujulisha umma Pamoja na wadau kwa ujumla juu ya changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa majukumu yetu ili kujenga uelewa wa Pamoja na hivyo kurahisisha utatuzi wa changamoto hizo.

Jarida hili ni kwa ajili ya umma wa Watanzania na wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi kujifunza na kutambua uwepo wa PSPTB kama Chombo kinachoweza kuangazia fursa zilizopo au zinazoweza kujitokeza kwaajili ya maendeleo ya kibiashara, changamoto za ununuzi na ugavi kukiwa na lengo la Pamoja la kujenga Uchumi imara wan chi yetu.

Kupitia jarida hili tutaunganisha sauti za wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi, watunga sera na watoa maamuzi Pamoja na walaji wa mwisho ambao ndio wanatoa mchango mkubwa katika ununuzi na ugavi hivyo kukuza Uchumi wetu

Jarida hili linachapishwa mara mbili kwa mwaka na linatumika kama kipaza sauti au jukwaa la usambazaji wa taarifa zinazohusu ununuzi na ugavi katika kupanua wigo wa uelewa kwa wadau na umma kwa ujumla.

Jarida hili pia linatarajiwa kuongeza thamani kwa shughuli za PSPTB kwa kujenga mawasiliano ya karibu na wadau waliopo na kuwavuta wapya kwenye mnyororo wa sekta ya ununuzi na ugavi ndani na njee ya nchi.

Malengo mengine ya jarida hili yatakuwa kuzijulisha sekta zingine za Uchumi kuhusu shughuli za PSPTB, kuwa jukwaa la kubadirishana Mawazo kwaajili ya kukuza sekta ya ununuzi na ugavi Pamoja na kutoa Habari sahihi kuhusu nafasi ya PSPTB katika kuikuza sekta hii muhimu

Tunatarajia kwamba wadau wa sekta bya ununuzi na ugavi Pamoja na wasomaji wote watakaofikiwa watatupa mrejesho utakaosaidia kuboresha jarida hili kwa manufaa ya maendeleo ya taifa katika kulinda maslahi ya nchi Pamoja



**Gedfred Mbanyi**
**Mkurugenzi Mtendaji**




## Bodi ya Uhariri

**Bi Shamim Mdee**
Mwenyekiti

**Beatrice Sanga**
Katibu

**Ikunda Erick**
Mhariri

**Dickson Mollel**
Mwandishi

**Wakili Hamza Twaha**
Mjumbe

**Boniface Mushi**
Mjumbe

# Matumizi ya kidigitali hayaepukiki sekta ya ununuzi na ugavi

**SERIKALI imesema ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kidijiti duniani, sekta ya ununuzi na ugavi haina budi kuyakumbatia matumizi hayo katika shughuli zake za kila siku ikiwemo usajili na uombaji wa zabuni mbalimbali.**



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Doto Biteko (Mb.) akihutubia washiriki wa Kongamano la 15 la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) Jijini Arusha.*





Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dk Dotto Biteko alisema hayo Desemba 17,2024 wakati akifungua Kongamano la 15 la Bodi ya Watalaam wa Ununuzi na Ugavi nchini (PSPBT) lililofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Kaulimbiu ya kongamano hilo ni 'Mabadiliko ya Ununuzi na Ugavi kwa Usimamizi Bora wa Rasilimali'.

Alisema kaulimbiu hiyo inaendana na mabadiliko ambayo serikali imeendelea kuyafanya ikiwemo matumizi ya mfumo wa manunuzi na ugavi wa kieletroniki (NeST) ambao umesaidia kutoa huduma bora na ya haraka zaidi.

"Napongeza mfumo wa usajili wa watalaam wa ununuzi na ugavi kwa njia ya mtandao unasomana na mfumo wa NeST, mfumo huu utahakikisha shughuli za ununuzi na ugavi zinafanywa na watu wenye sifa stahiki waliosajiliwa na PSPTB, hatua hii pia itasaidia kwenye udhibiti wa weledi na watalaam wanaotumia mfumo huu na waliosajiliwa na bodi,"alisema Dk Biteko .

Hivyo alisisitiza wasimamizi wa sekta hiyo kuongeza weledi na kuwaondoa watumishi wasio na vigezo.

Dk Biteko alisema serikali kupitia bajeti kuu ya serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitoa dira ya kuhakikisha ununuzi unafanyika kwa njia ya mtandao na kwa kuzingatia bei ya soko.

Hatua hiyo ni kupunguza gharama katika sekta ya manunuzi ya umma na kuleta tija kwa Watanzania na taifa kwa ujumla, hivyo kila sekta imetakiwa kuendana na dira hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya PSPTB, Benezeth Ruta alisema bodi hiyo inapaswa kuongezewa nguvu ya rasilimali watu ili kuendana na kasi ya matumizi ya teknolojia na kuondokana na ubadhilifu ambao umekuwa ukifanywa na baadhi ya watumishi wasio na weledi wa masuala ya ununuzi na ugavi.

Alisema hatua hiyo ni hatari kitaaluma kwa sababu hauleti tija katika eneo la ununuzi na ugavi na matokeo yake ni kusababisha upotevu wa fedha za umma.

"Mabadiliko ya kidijiti hayakwepeki katika dunia ya leo, katika ukaguzi unaoendelea PSPTB imebaini kuna upungufu mkubwa wa wataalam wenye sifa stahiki hususani katika halmashauri za miji, wilaya na manispaa nchini,"alisema Ruta.

Alisema upungufu huo umesababisha baadhi ya halmashauri na taasisi za umma kutumia watumishi wasio na sifa za taaluma hiyo kufanya kazi za manunuzi ya ugazi jambo ambalo ni nje ya taaluma hiyo na ni kinyume na kifungu cha 11 cha sheria ya PSPTB.

Kongamano hilo limewakutanisha wadau mbalimbali katika sekta ya ununuzi na ugavi nchini kutoka sekta ya umma na binafsi.




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande (Mb.) akihutubia washiriki wa Kongamano la 15 la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) Jijini Arusha.*

# Sekta ya ununuzi na ugavi yasisitizwa uzalendo na uadilifu

**WATAALAMU wa ununuzi na ugavi nchini wamesisitizwa kulinda maadili ya kazi na kusimamia upatikanaji wa haki kwa wote na kuepuka kutoa zabuni kwa upendeleo na rushwa kwenye miradi ya maendeleo.**

Naibu Waziri wa Fedha,Hamad Chande Hamad alisema hayo wakati akifunga Kongamano la 15 la Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi nchini (PSPBT) lililofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Aliwataka wataalamu hao kutumia vyema taaluma zao kuleta tija katika manunuzi mbalimbali ya umma.

Alisema sekta hiyo inapaswa kusimamia utoaji huduma bora kwa Watanzaniana kufanya ununuzi unaozingatia thamani ya fedha, upatikanaji wa vifaa na malighafi ambazo zimekuwa zikitumika katika miradi mbalimbali nchini.

"Ndugu zangu washiriki wa kongamano hili naomba mtambue serikali haitamvumilia yeyote atakayeshiriki vitendo visivyo vya kimaadili na kitaaluma, tutachukua hatua kali,tunawaasa muwe waadilifu na tekelezeni majukumu yenu inavyopaswa,"alisisitiza Chande.

Kadhalika aliwataka washiriki hao kuendana na matumizi ya mifumo ya kieletroniki ambayo imeendelea kuanzishwa na serikali ili kuepuka upotevu wa rasilimali fedha pamoja na ubadhilifu katika ununuzi na ugavi serikalini.

Nimefarijika sana kusikia mada kuu ya kongamano ikijielekeza kujadili mabadiliko ya kdigiti, naamini majadiliano mliyofanya yataleta tija katika kuboresha mfumo wa ununuzi na ugavi kwa njia ya mtandao."aliongeza Chande.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB, Benezeth Ruta alisema mada zilizowasilishwa katika kongamanio hilo ikiwemo, kujenga uchumi shindani kupitia mnyororo wa ununuzi na ugavi zitaleta mabadiliko na utendaji wenye tija kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

"Ni jukumu la kila mmoja wetu kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia maadili ili tuweze kuifikisha nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda na kuleta maendeleo ya wananchi wa taifa, bodi tunatoa rai kwa watalaamu wetu wote muwe wazalendo katika kutimiza wajibu wenu,'' alisema Ruta.

Kongamano hilo la 15 la mwaka la wataalamu wa ununuzi na ugavi lilianza Desemba 17,2024 na kufikia tamati Desemba 19,mwaka huo mjini Arusha.

Liliwakutanisha zaidi ya washiriki 1,800 wa sekta hiyo kutoka idara na taasisi mbalimbali za serikali pamoja na sekta binafsi.

Mada mbalimbali katika kongamano zilijadiliwa ikiwemo kubainisha vichocheo na vikwazo vya mabadiliko ya mnyororo wa ununuzi na ugavi, nafasi ya ununuzi na ugavi kwa usimamizi bora wa rasilimali, usimamizi wa miradi inayofadhiliwa kupitia mabadiliko ya ununuzi na ugavi.

# Wahitimu wa ununuzi na ugavi wahimizwa kujisajili kidijiti

**WAHITIMU wa masomo ya ununuzi na ugavi nchini wamehimizwa kujisajili kidijiti ili waweze kufanya mitihani ya kitaaluma pamoja na kutambulika kitaaluma.**

Hayo yalibainishwa Mei mwaka huu na viongozi wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi nchini (PSPTB) waliotembelea vyuo vinavyotoa mafunzo hayo katika mikoa mitatu nchini .

Bodi hiyo imewahimiza zaidi wanafunzi kujisajili kwa njia ya mtandao hususani kuwa mwanachama wa bodi hiyo lakini pia wajisajili ili waweze kufanya mitihani ya bodi ambayo hutolewa kwa wanachama wake.

> "Matakwa ya sasa ya ajira kwa kada ya ununuzi na ugavi lazima muombaji awe anatambulika na bodi ya ununuzi kwa hiyo tunaamini kwamba wanafunzi wetu wameelewa na watakuwa watiifu



*Maafisa kutoka Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) wakiwa kwenye picha ya Pamoja na wakufunzi wa masuala ya Ununuzi na Ugavi katika chuo cha Bandari jijini Dar es Salaam. Ambapo PSPTB ilitembelea chuo hicho ili kutoa elimu kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya ununuzi na Ugavi.*



*Wanafunzi wanaosoma taaluma ya ununuzi na ugavi kutoka chuo Bandari, Dar es Salam wakifuatilia mada mbalimbali zinazotolewa na maafisa kutoka Bodi ya Wataalam wa ununuzi na Ugavi PSPTB mara walipotembelea chuoni hapo kwa ajili ya kutoa elimu juu ya masuala ya usajili wa wataalam, Mitihani ya Bodi na kazi mbalimbali zinazofanywa na Bodi.*

Vyuo vilivyotembelewa ni vya mkoani Dar es Salaam, Morogoro na Iringa na ziara hiyo ni utekelezaji wa mpango mkakati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 unaohamasisha wanataaluma wa fani hiyo kujisajili na kutambuliwa.

Mkufunzi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Dk Julieth Kwashuma alisema mafunzo yaliyotolewa kupitia ziara hiyo yataendelea kuwaweka wanafunzi karibu na bodi hiyo ili kurahisisha kujifunza na kupata huduma mbalimbali zitolewazo na bodi hiyo.

"Matakwa ya sasa ya ajira kwa kada ya ununuzi na ugavi lazima muombaji awe anatambulika na bodi ya ununuzi kwa hiyo tunaamini kwamba wanafunzi wetu wameelewa na watakuwa watiifu na elimu hii itawasaidia kwenda kulijenga taifa letu,"alisema Dk Kwashuma.

Ziara hiyo ilikuwa na malengo yake ni kuongeza idadi ya wataalamu wa sekta ya ununuzi na ugavi waliosajiliwa, kuhimiza wanafunzi wanaohitimu masomo yao kujisajili kwa ajili ya mitihani ya kitaaluma pamoja na uanachama.

Aidha ziara hiyo ililenga kuimarisha uhusiano kati ya PSPTB na vyuo vilivyopo chini yake.

Vyuo vilivyotembelewa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), (Dar es salaam), Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA), Chuo cha Teknolojia cha Kilimanjaro (KITM) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)-Dar es Salaam.

Mkoani Morogoro vyuo vilivyotembelewa na viongozi wa PSPTB ni pamoja na Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro (MUM) na Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Iringa walitembelea Chuo Kikuu cha Mkwawa na Chuo Kikuu cha Tumaini.

Katika vyuo hivyo zaidi ya wanafunzi 1,000 wanaosoma fani hiyo kuanzia ngazi ya Astashahada,Stashahada na Shahada walipata mafunzo ushauri huo.

# Mbanyi: Baraza la Wafanyakazi kiungo muhimu mahali pa kazi




*Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB Bw. Godfred Mbanyi akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi PSPTB kilichofanyika katika ukumbi qa SUA mkoani Morogoro tarehe 9-10 Januari 2025*

**BODI ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB)imesema Baraza la Wafanyakazi mahali pa kazi ni chombo muhimu kinachowaunganisha wafanyakazi na mwajiri katika kusukuma maendeleo ya taasisi mbele.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya PSPTB, Godfred Mbanyi alisema hayo wakati wa ufunguzi wa baraza la wafanyakazi wa bodi hiyo lililokutana kujadili mafanikio,changamoto na jinsi ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo.

"Umuhimu wa mabaraza ya kazi mahali pa kazi, kwanza yanaleta ushirikishwaji wa wafanyakazi hatua inayowafanya wawe sehemu ya maamuzi katika taasisi,"alisema Mbanyi.

Kikao hicho kimefanywa ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizojitokeza wakati wa uandaaji wa bajeti kwa mwaka wa ujao wa fedha wa 2025/2026.

Mbanyi alisema baraza la wafanyakazi mahali pa kazi ni chombo kinachoundwa na sheria ya mahusiano kazini kwa ajili na kuweka mazingira mazuri mahali pa kazi na kinapaswa kuwa na mkataba baina ya menejimenti na chama cha wafanyakazi sehemu ya kazi.

Alisema kikao hicho pia kimefanywa kutathmini utendaji kazi wa bajeti ya mwaka ujao wa fedha wa 2025/2026 ambayo kwa mujibu wa sheria, bajeti yoyote kabla ya kuanza kutumika inapaswa iidhinishwe na baraza la wafanyakazi mahali pa kazi.

Mbanyi alisema bajeti ya mwaka 2024/2025 inakamilika Juni 30, 2025 hivyo ni wajibu wa menejimenti kulieleza baraza hilo mafanikio,changamoto na njia za utatuzi na vipaumbele vya bajeti ijayo.




*Menejimenti ya PSPTB wakiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wa PSPTB kwenye picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa kikao cha baraza hilo kilichofanyika katika ukumbi wa SUA mkoani Morogoro tarehe 9-10 January 2025*

# Wanataaluma ununuzi na ugavi wa TAA wapigwa msasa

**WATUMISHI 84 wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) wamepewa mafunzo ya Sheria Mpya ya Ununuzi na Ugavi ya mwaka 2023 na kanuni mpya za mwaka 2024 yanayowajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa weledi.**

Mafunzo hayo yameendeshwa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) na kufanyika katika ukumbi wa Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Abdul Mombokaleo alisema mafunzo hayo yamewasaidia watumishi hao kujiamini katika kutekeleza majukumu yao kwa maslahi ya taifa.

Mombokaleo alisema ili kusaidia wanataaluma hiyo kazini wamedhamiria kuendelea kuwapa mafunzo ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi kwa lengo la kuwajengea uwezo na ufahamu wa kusimamia miradi mbalimbali ya taasisi.

Mkurugenzi wa Huduma za Uanachama na Taaluma wa PSPTB, CPSP(T) Amos Kazinza alisema wametoa mafunzo hayo kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 na kanuni mpya za mwaka 2024.

Alisema jumla ya watumishi 84 wa sekta ya ununuzi na ugavi wa TAA kutoka kanda mbalimbali za mamlaka hiyo wamenufaika na mafunzo hayo.

"Sheria ya ununuzi na ugavi imekuwa na mabadiliko mengi ambayo inawataka wajumbe bodi ya zabuni waweze kuidhinisha baadhi ya manunuzi kulingana na ukomo wa uidhinishaji,"alisema CPSP(T) Kazinza. Pia alibainisha kuwa katika mabadiliko ya sheria hiyo inamtaka mhasibu aawajibike kuidhinisha manunuzi kulingana na ukomo wa uidhinishaji.

Katika sheria hiyo pia inawataka wataalamu wa ununuzi na ugavi kufanya ugavi, awali lilikuwa kwenye sheria ya fedha na kuwa baada ya sheria kufanyiwa marekebisho wataalamu hao wana jukumu la kufanya ununuzi na ugavi ili kuhakikisha mnyororo wa ugavi unasimamiwa vizuri.

"PSPTB inawajibu wa kuhakikisha kwamba wadau wote wanaosimamia ununuzi na ugavi wanapata uelewa wa pamoja ili kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana kwa kila mradi unaotekelezwa na taasisi au mamlaka,"alisema CPSP(T) Kazinza.

Kazinza ametoa wito kwa taasisi za umma na binafsi ya kuona fursa hii ya kuwajengea uwezo wataalamu wao kwasababu ya sehemu kubwa ya matumizi ni ununuzi.



*Mkurugenzi Mkuu kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Bw. Abdul A. Mombokaleo akifunga mafunzo juu ya sheria mpya ya Ununuzi na Ugavi ya mwaka 2023 na kanuni mpya za mwaka 2024 yaliyolenga kuwajengea uwezo wataalam wa Ununuzi na Ugavi kutoka TAA ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi.*



*Baadhi ya maafisa Ununuzi na Ugavi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), wakifuatilia mafunzo juu ya sheria mpya ya Ununuzi na Ugavi ya mwaka 2023 na kanuni mpya za mwaka 2024 yenye lengo la kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi.*

# PSPTB yaendesha mitihani 30 ya kitaaluma

**BODI ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) imeendesha mitihani yake ya 30 kwa watahiniwa zaidi ya 1,000 katika ngazi za tofauti za taaluma hiyo.**

Akizungumzia mitihani hiyo iliyofanywa katika mikoa saba nchini Mei mwaka huu, Afisa Mitihani wa PSPTB, Faraja Mgulambwa alisema mitihani hiyo imefanywa katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Mwanza na Zanzibar kati ya Mei 12 hadi 16,mwaka huu.

Alisema ili kupata sifa za kitaaluma ni lazima wahitimu kutoka vyuo mbalimbali wajisajili na kufanya mitihani ya bodi ili kupata vigezo vya kufanya kazi hiyo.

Faraja aliwasisitiza waajiri kutoajiri watumishi wa manunuzi na ugavi wasio na sifa stahiki hususani wale ambao hawajafanya mitihani ya kitaaluma na kuwa na ujuzi na maarifa stahiki.

"Bodi iko macho na hatua stahiki za kisheria na kimaadili zitaendelea kuchukuliwa kwa wale wanaokiuka sheria, kanuni na matakwa ya maadili ya utendaji kazi,"alisema Faraja.

Alisema hatua hizo zitachukuliwa kwa wataalam wa fani hiyo na wengine wote wanafanya kazi za ununuzi na ugavi bila kuwa na sifa stahiki ambazo ni pamoja na kusajiliwa bodi na kufanya mitihani.

Hivyo alitoa mwito kwa wanataaluma hao ambao bado hawajajisajili wafanye hivyo na kufanya mitihani ya bodi itakayofanyika Novemba mwaka huu.

Pia aliwasisitiza waajiri wenye watumishi wanaopaswa kufanya mitihani ya kitaaluma ili kuwa sifa zinazohitajika, wawape ruhusa watumishi hao ili waweze kujiendeleza na kuwalipia ada za mafunzo na mitihani ya kitaaluma.







# Wanafunzi UDSM wahamasishwa kuchangamkia fursa



**WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)kozi ya Ununuzi na Ugavi wamehamasishwa kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta hiyo ili waweze kujiajiri au kuajiriwa katika taasisi mbalimbali.**

Ushauri huo umetolewa na Meneja wa Mitaala wa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Jeremiah Haule, wakati akizungumza na wanafunzi hao waliofanya ziara ya mafunzo kuhusu bodi hiyo mkoani Dodoma.

Haule alisema wanafunzi wanapaswa kufahamu na kutumia fursa mbalimbali zilizopo kwenye sekta hiyo ili wanufaike na taaluma hiyo.

Alisema sekta hiyo ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi, kwa sababu inatoa nafasi nyingi za ajira ajira serikalini na katika sekta binafsi.

Aidha, alibainisha sekta hizo mbili zinategemea wataalamu wa ugavi waliothibitishwa na kusajiliwa na bodi hiyo hivyo ni muhimu kwa wanafunzi kuzingatia viwango vya taaluma na maadili ya kazi ili kuwa na ushindani katika soko la ajira.

Baada ya mafunzo hayo, wanafunzi walipata fursa ya kuzungumza na kueleza maoni yao kuhusu sekta ya hiyo pamoja na changamoto wanazokutana nazo katika masomo yao.

# Wanafunzi 243 wanufaika na mafunzo ya tafiti




**WANAFUNZI zaidi ya 243 wa fani ya ununuzi na ugavi kutoka mikoa mitano nchini wamepata mafunzo na mbinu maalum za kuwaandaa kuandika andiko la tafiti zitakazoleta matokeo chanya kwa sekta hiyo.**

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB),Godfrey Mbanyi alisema mafunzo hayo ni moja ya matakwa ya fani hiyo kwa wanataaluma wa sekta hiyo.

"Takwa mojawapo kwa wanafunzi hawa ni kuhudhuria semina na kupata mafunzo yatakayowapitisha kwa usahihi katika safari yao ya kufanya tafiti na kuhitimu vyema mafunzo hayo wakiwa wamepikwa na kuiva vizuri,"alisema Mbanyi.

Wanafunzi hao ni kutoka Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza na Dar es Salaam.

Alisema katika mafunzo hayo wanafunzi hao wanajengewa uwezo wa kuandika tafiti na ripoti mbalimbali kwa kufuata kanuni na miongozo ya PSPTB.

Mbanyi alisema kupitia mafunzo hayo wanafunzi wataelekezwa na kujengewa uwezo wa jinsi ya kuandaa andiko la utafiti hususani ya PSPTB ili waweze kuhitimu mafunzo hayo.

Mafunzo hayo ya siku tano yalifanywa Aprili 24 hadi 28,mwaka huu na kuwashirikisha wanafunzi zaidi ya 243 kutoka mikoa tajwa.



Watahiniwa wa mitihani ya 30 ya PSPTB wakiwa katika chumba cha mtihani katika ukumbi wa Suma JKT Jijini Dar es Salaam



Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wa PSPTB kwenye picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa kikao cha baraza hilo kilichofanyika katika Ukumbi wa SUA mkoani Morogoro tarehe 9-10 Januari 2025



Mkurugenzi wa Huduma za Uanachama na Taaluma wa PSPTB, CPSP(T) Amos K. Mang'ombe akitoa mada wamafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa ununuzi kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam



*Watahiniwa wa mitihani ya 30 ya PSPTB wakiwa katika chumba cha mtihani katika ukumbi wa Suma JKT Jijini Dar es Salaam*

*Afisa Ununuzi kutoka Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) Bw. Ally Mbarook akifafanua jambo kwa wanafunzi wanaosoma taaluma ya ununuzi na ugavi kutoka chuo cha Kilimanjaro Institute of Technology kilichopo Mwenge jijini Dar es Salaam*





*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB Ndg. Jacob Kibona (katikati) akiwa kwenye opicha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Bodi hiyo baada ya kikao cha kupitisha matokeo ya 30 ya mitihani ya PSPTB katika ukumbi wa jengo la Takwimu Juni 20, 2025*



**CPSP(T) Amani R. Ngonyani**
– Mkurugenzi wa Mitihani na Mafunzo ya Kitaaluma

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi kupitia kifungu cha 7 (e) na (f) cha Sheria ya PSPTB No. 23 ya mwaka 2007 imeanzisha mafunzo maalum ya kuandaa wakaguzi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi. Mafunzo haya pamoja na kukidhi matakwa ya Sheria tajwa pia yameanzishwa ili kutekeleza mwongozo wa usajili wa PSPTB wa kusajili wataalam wa ukaguzi katika tasnia ya ununuzi na ugavi.

Malengo mahusus ya mafunzo ya ukaguzi katika tasnia ya ununuzi na ugavi yamejikita kuwawezesha washiriki; kupata ujuzi na mbinu za ukaguzi katika utendaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi, kujua kanuni za maadili na viwango vya taaluma ya ukaguzi, kutambua sifa za kupata ithibati na usajili wa wakaguzi wa ununuzi na ugavi, kuimarisha weledi na utendaji wa kitaalamu katika ukaguzi wa tasnia ya ununuzi na ugavi, kutoa fursa kwa wahitimu kuanzisha kampuni za shughuli za ukaguzi katika tasnia ya ununuzi na ugavi katika sekta ya umma na binafsi na kukuza stadi za uongozi katika timu za ukaguzi na utamaduni wa kujitegemea.

Mafunzo ya ukaguzi yamefanyika katika awamu mbili katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mafunzo ambapo jumla ya washiriki 131 wamepatiwa mafunzo. Bodi ina Imani kubwa na weledi na uwepo wataalam hawa na kwamba kwa kushirikiana na mamlaka zingine nchini, uwepo wao utasaidia sana utendaji na ufanisi wasekta ya Ukaguzi na hususani eneo la Ununuzi na Ugavi.

**MITHANI YA 30 YA PSPTB**

Bodi katika kutekeleza majukumu yake imeendesha mitihani ya Taaluma ya Ununuzi na Ugavi nchini kuanzia tarehe 12.05.2025 mpaka tarehe 16.05.2025 katika vituo saba vilivyoko katika mikoa ya Dar Es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro na Mbeya na kimoja kikiwepo Zanzbiar.

Jumla ya watahiniwa 1,464 walidahiliwa kufanya mitihani hii kuanzia ngazi ya stashahada ya taaluma ya ununuzi na ugavi mpaka hatua ya utafiti (research).



**CPSP(T) Amos K. Mang'ombe**
-Mkurugenzi wa Huduma za Uanachama na Taaluma

Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), kupitia Kurugenzi ya Maendeleo ya Taaluma(DPD), ina jukumu la msingi la kusimamia na kuendeleza ubora wa taaluma ya ununuzi na ugavi nchini. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Kurugenzi hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa kupitia shughuli mbalimbali zikiwemo usajili wa wanachama wapya, utoaji wa mafunzo ya kitaaluma, utoaji wa huduma za ushauri elekezi na uratibu wa kongamano la mwaka la wataalamu wa ununuzi na ugavi.

**1. USAJILI WA WANACHAMA**

Tangu kuanzishwa kwa PSPTB mwaka 2007, jumla ya wanachama 18,544 wamesajiliwa rasmi. Wanachama hawa wamegawanyika katika madaraja mbalimbali kulingana na vigezo vya kitaaluma vilivyowekwa na Bodi. Wanachama 1,026 wamesajiliwa katika daraja la Authorized (AU), 1,610 katika daraja la Approved (AP), 11,263 katika daraja la Graduate (GP), 4634 wamesajiliwa katika Daraja la Technician (TE). Aidha, taasisi 10 zimesajiliwa kama Tuition Providers na kampuni moja ya ushauri (Consulting Firm) nayo imesajiliwa rasmi. Takwimu hizi zinaonesha kuwa PSPTB imepiga hatua kubwa katika kujenga msingi imara wa wataalamu waliothibitishwa kitaaluma.

**2. MAFUNZO YA MAENDELEO YA TAALUMA (CPD) NA MAFUNZO YA NDANI (TAILOR-MADE TRAINING)**

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, PSPTB imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kukuza ujuzi wa wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini. Mafunzo haya yalihusisha warsha (CPD workshops), mafunzo ya ndani (tailor-made training), huduma za ushauri elekezi, na kongamano la mwaka 2024.

Katika kipindi husika, PSPTB iliendesha jumla ya warsha 20 na mafunzo ya ndani 19. Mafunzo haya yalihudhuriwa na jumla ya washiriki 1,603, idadi ambayo ni zaidi ya lengo la awali la washiriki 1,000. Hii ni sawa na asilimia 160 ya lengo na ni kielelezo cha mwitikio mkubwa kutoka kwa wataalamu wa taaluma hii katika kujifunza na kuongeza maarifa yao ya kazi.

**3. HUDUMA ZA USHAURI ELEKEZI**

PSPTB ilitoa huduma za ushauri elekezi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambapo wafanyakazi 150 walihudhuria mafunzo na ushauri uliotolewa. Ushauri huu ulikuwa na lengo la kusaidia taasisi hiyo kuboresha mfumo wake wa ununuzi na ugavi kwa kuzingatia sheria, kanuni, na viwango bora vya kitaaluma.

**4. KONGAMANO LA MWAKA LA WATAALAMU WA UNUNUZI NA UGAVI LA 15**

PSPTB iliratibu kwa mafanikio makubwa Kongamano la 15 la mwaka la wataalamu wa ununuzi na ugavi lililofanyika katika ukumbi wa AICC, Arusha, kuanzia tarehe 17 hadi 19 Desemba 2024. Kongamano hilo lilikuwa na kaulimbiu isemayo: "Mabadiliko ya Ununuzi na Mnyororo wa Ugavi kwa Usimamizi Bora wa Rasilimali (Procurement and Supply Chain Transformation for effective Management of Resources)."

Kongamano hili liliwakutanisha wataalamu wa kada mbalimbali za ununuzi na ugavi kutoka sekta ya umma na binafsi, wataalamu wa taaluma, washauri, na wadau wengine. Jumla ya washiriki 1,981 walihudhuria kongamano hilo, ikiwa ni asilimia 99.05 ya lengo la washiriki 2,000 waliokuwa wamepangwa.

Lengo kuu la kongamano hilo lilikuwa ni kuhamasisha mijadala ya kitaaluma, kuendeleza utafiti, kubadilishana uzoefu na kushauri maboresho ya mifumo ya ununuzi na ugavi katika taasisi mbalimbali nchini.

**5. TAARIFA YA UKAGUZI WA TAASISI ZA UMMA NA BINAFSI**

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, PSPTB ilifanya ukaguzi wa taasisi za umma na binafsi katika mikoa 13, ambapo taasisi 227 zilifanyiwa tathmini ya uzingatiaji wa sheria ya usajili wa wataalamu. Jumla ya watumishi 1,120 waliokuwa wakitekeleza majukumu ya ununuzi na ugavi walibainika, kati yao 1,008 walikuwa wamesajiliwa rasmi na PSPTB, huku 113 wanafanya kazi hizo bila kusajiliwa na PSPTB. PSPTB imeanza kuchukua hatua stahiki dhidi ya wote waliobainika kukiuka masharti ya sheria kwa lengo la kuimarisha uadilifu na weledi katika taaluma ya ununuzi na ugavi nchini.

**HITIMISHO**

Kupitia mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2024/2025, Kurugenzi ya Maendeleo ya Taaluma ya PSPTB inaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha taaluma ya ununuzi na ugavi inaendelezwa kwa mujibu wa viwango vya kitaaluma vya kimataifa.



**Bi. Grace A. Mselle**
Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA

Katika nafasi yangu kama Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA katika Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), niliongoza mchakato wa mageuzi ya kidijitali uliolenga kuboresha huduma za usajili na uthibitisho wa kitaaluma. Mnamo mwaka 2017, tulibaini ucheleweshaji mkubwa na kutoendana kwa ufanisi katika taratibu zetu za usajili na uthibitisho wa kitaaluma zilizokuwa zikifanywa kwa mikono, hali iliyokuwa ikidhoofisha utoaji wa huduma na kuridhika kwa wadau.

Kama hatua ya kukabiliana na changamoto hizi, kufikia Septemba 2019, PSPTB ilizindua mfumo wa mtandaoni wa usajili na uthibitisho wa kitaaluma (https://registration.psptb.go.tz/), ambao ulibadilisha taratibu za kutumia karatasi na kuongeza ufanisi kwa kiasi kikubwa.

Hatua muhimu zilizochangia mafanikio haya zilijumuisha tathmini ya kina ya mahitaji ikihusisha idara mbalimbali ili kubaini mahitaji ya mfumo. Niliratibu na kusimamia timu ya wataalamu wa fani mbalimbali wakiwemo watengenezaji wa mfumo, wamiliki wa michakato, na washauri wa nje. Mfumo huu uliwawezesha waombaji kufuatilia hali ya usajili wao kwa wakati halisi. Ili kuwezesha malipo ya kidijitali, tuliunganisha mfumo na njia za malipo kupitia benki na simu za mkononi kupitia Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki (GePG).

Matokeo yalikuwa makubwa: muda wa kushughulikia maombi ulipungua kutoka wiki tatu hadi chini ya siku tano, na upatikanaji wa huduma uliongezeka kwa asilimia 70%, hasa kwa wataalamu walioko nje ya Dar es Salaam na Dodoma. Maoni baada ya utekelezaji yalionyesha kuridhika zaidi kwa wateja. Mradi huu uliinua hadhi ya PSPTB kama taasisi ya umma inayobuni na kuweka mfano kwa taasisi nyingine za udhibiti nchini Tanzania.

Kama Mkuu wa Kitengo, nina jukumu la kuoanisha mikakati ya TEHAMA na malengo mapana ya PSPTB. Majukumu yangu ni pamoja na kuongoza juhudi za mabadiliko ya kidijitali, kuelekeza mipango ya TEHAMA, na kukuza utamaduni unaoendeshwa na teknolojia katika idara zote. Kwa kuendesha mchakato wa kiotomatiki na kidijitali, tunarahisisha upatikanaji wa data kwa wakati halisi na kufanya maamuzi bora—kuimarisha nafasi ya PSPTB kama mdhibiti mwenye mtazamo wa mbele.

Kwa maelezo zaidi kuhusu mfumo wa usajili wa mtandaoni wa PSPTB, tafadhali tembelea: https://registration.psptb.go.tz/.



**Wakili Piencia Kiure**
Mkuu wa Kitengo cha Huduma za sheria

Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Kitengo cha huduma za Sheria cha Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), kimeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha kuwa shughuli zote za kitaasisi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na maadili ya taaluma ya ununuzi na ugavi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi 2024/2025, Kitengo katika utendaji kazi wake kinazingatia maeneo makuu manne ambayo ni: usimamizi wa mikataba, uimarishaji wa ushirikiano wa kitaasisi kupitia mikataba ya makubaliano (MoUs), usimamizi wa maadili ya kitaaluma, pamoja na mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya PSPTB ili kuendana na mazingira ya sasa ya kitaaluma.

### 1. Mikataba na Makubaliano ya Kitaasisi

